**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

# TANGAZO LA NAFASI ZA MAFUNZO YA UALIMU

## NGAZI YA STASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA SEKONDARI KWA MWAKA WA MASOMO 2023/2024

### UTANGULIZI

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia anatangaza nafasi za mafunzo ya Ualimu kwa ngazi ya Stashahada ya Ualimu ya Sekondari. Waombaji wa mafunzo haya ni wahitimu wa Kidato cha SITA wenye ufaulu wa Daraja la Kwanza hadi la Tatu (I-III). Wizara inakaribisha maombi ya kujiunga na mafunzo ya Ualimu katika Vyuo vya Serikali na visivyo vya Serikali kwa kuzingatia sifa zilizobainishwa katika tangazo hili.

### SIFA ZA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UALIMU

Sifa za jumla za kujiunga na Mafunzo ya Ualimu Tarajali ngazi ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Sekondari ni wahitimu wa Kidato cha Sita wenye ufaulu wa Daraja la I-III kwa kiwango cha "Principal Pass" mbili (02) za masomo yanayofundishwa katika shule za sekondari kidato cha I-IV. Aidha kwa waombaji ambao moja ya "Principal Pass"mbili ni somo la Uchumi "Economics", wanaweza kuomba kozi za fani ambazo ni

Mchezo (Physical Education and sports), Muziki, Sanaa za Ufundi (Fine Arts), na Sanaa za Maonesho (Theatre and Performing Arts).

## AINA YA MAFUNZO NA SIFA

Jedwali lifuatalo linaonesha aina ya mafunzo ya Ualimu, sifa za kujiunga, vyuo vinavyotoa mafunzo hayo na muda wa mafunzo

### A. MAFUNZO YA UALIMU TARAJALI NGAZI YA STASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA SEKONDARI

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Stashahada ya Ualimu Sayansi na Hisabati | Ufaulu wa Kidato cha **VI** kwa kiwango cha daraja la **I-III** na alama zisizopungua 'Principal Pass' mbili katika masomo ya Tahasusi za Sayansi, Hisabati na TEHAMA kwa kuzingatia Masomo yanayofundishwa katika shule za Sekondari kama ifuatavyo: Basic Mathematics, Biology,Food &nutrition , Geography, Chemistry, Physics, Agriculture Science, Information and Computer Studies (ICS) na Computer Science. | Monduli TC, Mandaka TC, Butimba TC, Kleruu TC, Songea TC, Tukuyu TC, Kasulu TC, Mpwapwa TC, Morogoro TC, Korogwe TC, Mamire TC na Tabora TC | Maka 2 |
| 2 | Stashahada ya Sayansi ya Jamii , Biashara na Lugha | Ufaulu wa Kidato cha **VI** kwa kiwango cha daraja la **I-III** na alama zisizopungua 'Principal Pass' mbili kwa kuzingatia masomo yanayofundishwa katika shule za Sekondari Kidato cha **I-IV**. Masomo yanayofundishwa katika shule za Sekondari kidato cha **I-IV** ni : Kiswahili, English, History, Geography, Civics, Commerce and Book keeping. | Bunda TC, Mtwara (K) TC, Marangu TC, Nachingwea TC, Shinyanga TC, Mandaka TC, Mpuguso TC, Dakawa TC, Butimba TC, Tabora TC, Morogoro TC, Tarime TC, Shinyanga TC, | Maka 2 |
| 3 | Stashahada ya Ualimu | Ufaulu wa Kidato cha **VI** kwa kiwango cha | Butimba TC | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Mchezo, Muziki, Sanaa za Ufundi na Sanaa za Maonesho | Daraja la **I-III** na alama zisizopungua 'Principal Pass' mbili pamoja na ufaulu wa masomo ya liyoainishwa katika mtihani wa kidato cha **IV** kwa kila kozi kama ifuatavyo | | Maka 2 |
| | | (a) **Sanaa za Ufundi**: masomo ya Fine Arts,Basic Mathematics, Chemistry, History, Physics, English na Civil Engineering**.** | Butimba TC | Maka 2 |
| | | (b) **Sanaa za Maonesho**: masomo ya English,Literature in English, Kiswahili, Geography na History. | Butimba TC | Maka 2 |
| | | (c) **Muziki**: masomo ya 'Music' pamoja na masomo ya English, Kiswahili, Physics, Geography, History na Biology. | Butimba TC | Maka 2 |
| | | (d) **Elimu kwa Mchezo**: masomo ya Physical Education and sports, Languages, na Biology. | Butimba TC na Mtwara (K) | Maka 2 |

## B. MAFUNZO YA UALIMU KAZINI (STASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA SEKONDARI)

| Na. | AINA YA MAFUNZO | SIFA ZA KUJIUNGA | CHUO | MUDA WA MAFUNZO |
|---|---|---|---|---|

| Na. | AINA YA MAFUNZO | SIFA ZA KUJIUNGA | CHUO | MUDA WA MAFUNZO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Stashahada Elimu Maalum (Mafunzo Kazini) Sekondari | Mwalimu kazini (aliyeajiriwa katika shule za Serikali au Shule binafsi) aliyepitia mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Astashahada, Stashahada au Shahada na mwenye uzoefu wa kazi ya Ualimu usiopungua miaka 2; Aidha awe aliyefaulu masomo ya Sayansi katika mtihani wa Kidato cha Sita | Patandi TC | Maka 2 |

**UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI**

(i) Tangazo hili linawahusu wahitimu wote wa kidato cha sita.

(ii) Waombaji wa Mafunzo ya Ualimu katika vyuo vya Ualimu vya Serikali wanatakiwa kujisajili na kufanya maombi **kielektroniki kupitia tovuti (tcm.moe.go.tz)**

(iii) Waombaji wa Mafunzo ya Ualimu kwa vyuo visivyo vya Serikali watume maombi yao moja kwa moja katika vyuo wanavyotaka kusoma na vyuo husika viwasilishe sifa za waombaji Baraza la Mtihani Tanzania kwa uhakiki.

(iv) Waombaji wa mafunzo ya Ualimu katika Vyuo vya Serikali watachagua tahasusi hadi tatu (03) kwa kuanza na ile anayoipenda zaidi

(v) Waombaji wa nafasi za mafunzo walio kazini wanapaswa kuwa wamehitimu mafunzo ya Ualimu ngazi ya Cheti, Stashahada au Shahada.

(vi) Walimu Kazini watapaswa kuambatisha barua ya ruhusa kutoka kwa waajiri wao;

(vii) Majibu kwa watakaochaguliwa kujiunga na Mafunzo ya Ualimu yatatolewa kupitia "**account**" aliyotumia mwombaji kuomba mafunzo ya

Ualimu, katika tovuti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na katika **Vyuo vya Ualimu walivyochaguliwa (kuanzia 05/08/2023).**

(viii) Barua na fomu za kujiunga na Mafunzo zitatolewa kupitia tovuti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (www.moe.go.tz) na Chuo atakachopangwa mwombaji kwa kutumia anuani yake. Waombaji wote wanashauriwa kuandika anuani kamili, barua pepe na namba ya simu inayopatikana kwa mawasiliano zaidi.

(ix) **Mwisho wa kutuma maombi kwa Mafunzo ya Ualimu ni tarehe 31/07/2021.**

**Tanbihi:** Masomo ya Dini hayatatumika kama kigezo cha sifa ya kujiunga na Mafunzo ya Ualimu

**Mawasiliano**

**Baruapepe:** info@moe.go.tz,

**Tovuti:** www.moe.go.tz

**Simu:** 026 2963533